Opération vaccination COVID-19

Sote tuna maswali muhimu ya kuuliza kuhusu chanjo.

Je, chanjo za COVID-19 ni salama?

Chanjo za COVID-19 zinazotolewa nchini Canada ni salama na faafu. Zimeidhinishwa na kamati ya wataalam wa kisayansi na madaktari wa Health Canada. Chanjo hizi zimezingatia viwango na usalama sawa vya ubora kama chanjo nyingine yoyote inayotumika Canada.

Nchi za Canada na mji wa Quebec zina mfumo thabiti wa ufuatiliaji wa chanjo.

Chanjo dhidi ya COVID-19 zina ufanisi kiasi gani?

Chanjo zote za COVID-19 zina ufanisi wa zaidi ya 80% dhidi ya ugonjwa mkali, kulazwa hospitalini na kifo. Ikiwa una maswali kuhusu chanjo, wasiliana na mtaalamu wa huduma ya afya anayekuhudumia katika kituo cha chanjo. Kisha utaweza kufanya uamuzi sahihi.

Kwa nini chanjo ni muhimu?

Chanjo dhidi ya COVID-19 huzuia ugonjwa mkali na hatari za matatizo ya baadaye. Lengo kuu la chanjo dhidi ya COVID-19 ni kupunguza kulazwa hospitalini na vifo vinavyohusiana na COVID-19 kwa wale walio katika hatari zaidi. Inapaswa pia kuchangia katika kudumisha huduma za afya na jamii na kuwezesha watu kurudi maisha ya kawaida haraka iwezekanavyo.

Ni nani aliye hatarini?

Wazee wako katika hatari zaidi ya kukumbwa na matatizo na kufa kutokana na COVID-19. Wale walio na magonjwa sugu, ambao hukaribiana mara kwa mara na watu walioambukizwa au kinga isiyo thabiti pia wako katika hatari, lakini umri ndio sababu kuu ya hatari

Ninaweza kuchanjwa wapi?

Unaweza kuchanjwa ukiwa au usipokuwa na miada. Ili kupata kituo kilicho karibu nawe na tarehe za chanjo, tembelaQuébec.ca/vaccinCOVID. Hutalipishwa ada zozote kupokea chanjo. Chanjo za COVID-19 hazitolewi katika vituo vya binafsi.

Je, na nikiwa na changamoto za kutumia mtandao?

Ikiwa unatatizika kutumia mtandao, omba usaidizi kutoka kwa familia au marafiki. Ikiwa huna muunganisho wa intaneti, piga simu kwa 1-877-644-4545 (nambari usiyolipishwa ada yoyote).

Je, ninaweza kupata chanjo hata ikiwa sina kadi ya bima ya afya?

Ikiwa wewe sio mkazi wa kudumu na huna kadi ya bima ya afya, bado unaweza kupokea chanjo ya COVID-19 kwa sababu hii ni hatua ya afya ya umma kulinda kila mkazi wa Quebec. **Unaweza kupokea chanjo, licha ya hali yako ya uhamiaji. Taarifa hii hutumiwa tu kubaini utambulisho wa watu kwenye sajili ya chanjo.** Hatutaituma kwa mamlaka au kuitumia kwa madhumuni mengine. Ikiwa huna kadi ya bima ya afya, piga simu kwa 1-877-644-4545 (nambari usiyolipishwa ada yoyote).

Je, ninahitaji dozi ngapi za COVID-19 ili kulindwa kabisa?

Inachukua angalau siku 14 ili dozi ya kwanza ianze kufanya kazi. Dozi ya pili ni muhimu ili kupunguza maambukizi zaidi na kuongeza kinga na kipindi cha kinga.. Dozi ya pili itaanza kufanya kazi baada ya wiki moja. Wiki moja baada ya kupokea dozi hii ya pili, utakuwa na kinga ya kutosha. Kwa kinga bora zaidi, dozi ya pili sharti itolewe ndani ya wiki nane au zaidi baada ya dozi ya kwanza.

Kwa watu ambao wamepata COVID-19 angalau siku 21 kabla ya kupokea chanjo, dozi moja ya chanjo ni muhimu. Maambukizi huchochea mfumo wa kinga kwa njia ile ile ambayo dozi ya kwanza wa chanjo itafanya. Kwa hivyo dozi ya chanjo anayopewa mtu aliye na COVID-19 itaimarisha kinga mwili kama vile dozi ya pili itakavyomlinda mtu ambaye hajawahi kuambukizwa. Kumbuka kuwa sio hatari kwa mtu ambaye ameambukizwa COVID-19 kupokea dozi mbili za chanjo.

Utapata miadi kurudi katika kituo cha chanjo ili uopkee chanjo yako.

Je, ninapokea uthibitisho wa chanjo?

Unapochanjwa mjini Quebec, utakabidhiwa nakala ya karatasi ya kuthibitisha kuwa umepokea chanjo. Hatua hii inatumika katika chanjo zote, ikiwa ni pamoja na chanjo za COVID-19. Utakabidhiwa pia thibitisho wa dijitali wa chanjo baada ya kupokea chanjo ya COVID-19. Uthibitisho huu wa chanjo ni faili

ya PDF ambayo unaweza kupakua kutoka kwenye kompyuta au simu yako. Hata ikiwa una uthibitisho wa chanjo wa dijitali, tunakushauri **sana** uhifadhi nakala ya karatasi ya uthibitisho wako.

Baada kupokea chanjo ya COVID-19, unaweza pia kupakua uthibitisho wako wa dijitali wa chanjo katika **tovuti ya kujihudumia**. Ili ufikie, nenda kwenye https://covid19.quebec.ca/PreuveVaccinale. Ukiwa kwenye tovuti, utaulizwa kutoa maelezo yafuatayo:

- Jina lako la kwanza na la mwisho;
- Tarehe yako ya kuzaliwa;
- Tarehe uliyopokea dozi ya kwanza ya chanjo ya COVID-19;
- Jina la chapa ya dozi ya kwanza ya COVID-19 uliyopokea:
- Nambari yako ya bima ya afya.

Baada ya taarifa hii kuthibitishwa, utaweza kupakua uthibitisho wako wa dijitali wa chanjo, isipokuwa ujumbe wa hitilafu unapotokea. Katika hali hiyo, hautaweza kupakua uthibitisho wako kwenye tovuti. Utaona ujumbe wa hitilafu ikiwa:

- Baadhi ya taarifa ulizotoa hazilingani na taarifa katika Sajili ya Chanjo ya Quebec au sajili ya Régie de l'assurance maladie du Québec (RAMQ).
- Wazazi wako hawajasajiliwa na RAMQ.

Tunaendeleza juhudi za kuhakikisha kuwa kila mtu anayechanjwa anapokea uthibitisho wa dijitali. Watu ambao wana umri wa chini ya miaka 14 hawataweza kupakua uthibitisho wao kupitia tovuti.

Ikiwa karatasi yako au nakala ya dijitali ya uthibitisho wako wa chanjo ina hitilafu, sharti zirekebishwe. Weka tu miadi kwenye Clic Santé mtandaoni kwa kuchagua Chanjo ya COVID-19 - Huduma ya utatuzi. Kisha sharti uende mwenyewe katika kituo cha chanjo ukiwa umebebea kadi yako ya bima ya afya au utambulisho mwingine.

Kwa maelezo zaidi kuhusu uthibitishaji wa chanjo, tembelea:
https://www.quebec.ca/en/health/health-issues/a-z/2019-coronavirus/progress-of-the-covid-19-vaccination/proof-covid-19-vaccination

Kumbuka: chanjo hupunguza dalili na kuzuia matatizo ya afya yanayohusiana na COVID-19. Chanjo ndiyo mfumo bora zaidi wa kinga.